



revised: 8/2018

Mkataba wa Afrika juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC)

Maelezo ya kirafiki ya watoto

Mwaka wa elfu moja mia tisa na tisini, Umoja wa Afrika uliandika Mkataba wa Afrika juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto ili kuongeza ulinzi zaidi kwa haki za watoto. "Haki" ni kitu ambacho kila mtoto anastahili kupata. Haki za mtoto mmoja haziwezi kuondoa haki za mtu mwingine. Wakati mtoto ni mdogo, watu wazima lazima wafanye maamuzi kwa mtoto. Watu wazima wanapaswa kuzingatia juu ya kile ambacho kinafaa kwa mtoto, si kile mtoto au mtu mzima anataka. Wakati mtoto anapozidi kukomaa, ana faa apewe uhuru zaidi na ataweza kufanya maamuzi zaidi juu ya haki zake.

Mtoto:

Mtoto ni mtu mdogo kuliko umri wa miaka 18. (Kifungu cha 2)

Watoto wote wana haki hizi, bila kujali wanavyoonekana, wapi wanaishi, ni dini gani au kabila gani wanapotoka, iwe ni wavulana au wasichana, au ni wazazi wao nini wanachofanya. (Kifungu cha 3)

Haki za watoto

Watoto wana haki ya:

- Kuishi na kukua. Watoto hawawezi kuuawa hata kama wamefanya uhalifu. (Kifungu cha 5)
- Wanafaa wapate jina na nchi. (Kifungu cha 6)
- Wanafaa waseme wanacho fikiria ata kama inaudhi wengine (Kifungu cha 7)
- Waungane pamoja katika vikundi ambazo ni za amani. (Kifungu cha 8)
- Waumini wa dini ambayo wanataka. Wazazi wanafaa kuwasaidia kujua maadili mazuri, ukweli na kisicho kuwa cha kweli. (Kifungu cha 9)
- Faragha. (Kifungu cha 10)
- Masomo ili kukuza talanta. Haya masomo yanafaa kujumuisha maadili na utamaduni wa kiafrika. Watoto wanafaa wafuzwe kuishi pamoja na watu wa tabaka na dini mbali mbali. Jinsi ya kutunza mazingira yao na kuwa na afya njema. (Kifungu cha 11)
- Kucheza na kufanya sanaa (Kifungu cha 12)
- Watoto wanafaa wapewe usaidizi maalum ili waweze kushiriki katika jamii na waweze kupata elimu wakati wana ulemavu. (Kifungu cha 13)
- Msaada wa dawa na maji safi ili waweze kuwa na afya njema. (Kifungu cha 14)

- Watoto wanafaa kuwa na hali salama za kufanya kazi. Watoto hawafai kutumiwa vibaya wakati wanafanya kazi. Hawafai kufanya kazi ambazo huwaumiza au kuwazuia kwenda shule au kukua ki akili na mwili. (kifungu cha 15)
- Kuthibitishwa kuwa na hatia ya uhalifu. Watoto waliofanya uhalifu hawawezi kuteswa au kuwekwa na wahalifu wazima. (Kifungu cha 17)
- Watoto wanafaa kuishi na wazazi wao kama hakuna hatari. Ikiwa mtoto haishi na wazazi wake, anafaa apewe mtu na wazazi wake (Kifungu cha 19)
- Kama watoto wametenganishwa na wazazi wao, wanafaa wapewe nyumba salama za familia mpaka watakapo ungana na familia zao (Kifungu cha 25)

Wajibu wa Watoto:

Watoto wana majukumu kwa jamii. Wanapaswa kuonyesha heshima kwa wazee, kusaidia kuunganisha na kuimarisha Afrika, na kufanya kazi kwa amani kwa kutumia vipaji vyao. (Kifungu cha 31)

Majukumu ya Wazee & Serikali:

Sheria hii ni muhimu zaidi kuliko desturi zote na mila ambayo inakabiliana na sheria hii. (Kifungu cha 1)

Watu wazima wanapaswa kufanya kile ambacho kinafaa kwa mtoto wakati wa kufanya uamuzi. Wanapaswa kuomba maoni ya mtoto. (Kifungu cha 4)

Ni wajibu wa wazazi kutunza watoto wao. (Kifungu cha 18)

Wazazi na serikali lazima watunze mahitaji ya mtoto wanapokua. Adhabu haiwezi kuwa na madhara kwa mtoto. (Kifungu cha 20)

Watu wazima na serikali lazima wawalinde watoto kutoka:

- Unyanyasaji au mateso (Kifungu cha 16)
- Mazoea ya jadi ambayo yanawaumiza watoto, kama ndoa ya watoto (Kifungu cha 21)
- Vita. Watoto hawawezi kuwa askari au kufanya kazi katika vita. (Kifungu cha 22)
- Utunzaji usiofaa (Kifungu cha 26)
- unyanyasaji wa kijinsia (Kifungu cha 27)
- Matumizi mabaya ya madawa ya kulevya na biashara ya madawa ya kulevya (Kifungu cha 28)

Serikali inapaswa kulinda watoto ambao wameacha nyumba zao kama wakimbizi. (Kifungu cha 23)

Child Protection Toolkit

Serikali na mashirika wanapaswa kupanga mpango wa watoto kwa uangalifu ili kuhakikisha kuwa watoto watakuwa salama na kupendwa katika familia zao mpya. (Kifungu cha 24)

Watoto hawawezi kuuzwa na mtu yeyote hata ikiwa ni wazazi wanataka. Watoto hawafai kufanya kazi kama waombaji. (Kifungu cha 29)

Watoto hawafai kuishi gerezani kwa sababu mama yao amefungwa. (Kifungu cha 30)